# “Bongo Fleva Inapotosha Jamii”: Je, ni Dai Jipya katika Maendeleo ya Fasihi ya Kiswahili?

*Method Samwel*

*Ikisiri*

Muziki wa Bongo Fleva umepitia kipindi kigumu cha kihistoria kwa kukataliwa na kuonekana kwa unapotosha jamii. Japo kwa sasa muziki huu unaonekana kukubalika, bado kuna baadhi ya watu wanauona kwamba unapotosha jamii. Miongoni mwa mambo yaliyoufanya muziki huu ukataliwe na kuhusishwa na upotoshaji wa jamii ni mavazi ya wasanii wake, maneno ya kihuni yanayotumika, tabia za wasanii, matumizi ya madawa ya kulevya, pombe na mengine ya aina hiyo. Makala haya yanapitia na kuangalia ikiwa dai kwamba kazi za fasihi hasa muziki wa Bongo Fleva unapotosha jamii ni jipya au la. Aidha, makala haya yanatoa mwelekeo mpya wa kufuatwa na wanajamii katika kuzihukumu kazi za fasihi za aina hiyo.

## 1.0 Utangulizi

Muziki wa Bongo Fleva (Bongo Flava) kwa upande mwingine huitwa pia muziki wa kizazi kipya (Suriano, 2006; 2007 na Omari, 2009) ikiwa na maana kwamba ni muziki unaopendwa sana na vijana ambao ndio hasa huonekana kuwa kizazi kipya au kizazi cha leo. Dhana ya muziki wa Bongo Fleva imekuwa na mkanganyiko mkubwa hasa katika jitihada za kuitofautisha na dhana ya *Hip hop* (Suriano, 2006; Omari, 2009; Samwel, 2011). Wapo wanaouona muziki huu wa Bongo Fleva kuwa ni aina mojawapo ya muziki wa *Hip hop* ya Kitanzania (Suriano, 2006 na 2007). Aidha, *http://spotistarehe.wordpress.com* ikiwa na mtazamo kama huo inaeleza kama ifuatavyo:

> Muziki wa Bongo Fleva unatofautiana na Genge (wa Kenya) kwani wao ni *Commercial* (***wa kibiashara***) zaidi wakilenga kuchezesha (***kuwaburudisha***) watu na wakati mwingine hupati maana kwenye wimbo mzima hata wakihojiwa wanashindwa kusema muziki ulilenga nini. Tofauti na muziki wetu (***Bongo Fleva***) ambao unalenga kutoa ujumbe na kuburudisha, ndio maana utaona kila mtu anajitahidi kumshirikisha mtu mwingine kwa ajili ya kuleta ladha tofauti ambayo pia inapatikana kwenye makundi, na utaona nyimbo nyingi ambazo mtu amemshirikisha mwingine zimewatoa sana (Ufafanuzi wetu).

Maelezo haya yanatudokeza kwamba *Hip hop* ni kundi kubwa la muziki duniani. Kila nchi ina mtindo wake. Kwa mfano, Kenya-Genge, Afrika ya Kusini-Kwaito, Tanzania-Bongo Fleva, na kadhalika.

Aidha, wapo wanaoutofautisha muziki wa Bongo Fleva na *Hip hop* kwa vigezo vya midundo na mapigo. Kwa mfano, Ramadhani Mponjika (p.h.k[1] Chief Rhymson), katika mahojiano yetu, alitueleza kwamba muziki wa Bongo Fleva ni "kapu" ambapo ndani yake kuna muziki wa aina mbalimbali ikiwemo *zouk*, *rhumba*, *reggae*, *RnB* na kadhalika. Aidha, anadai kwamba mapigo ya muziki huu huwa ni mepesi. Akiielezea *Hip hop* anasema ni muziki unaofanana kote duniani na una mapigo mazito (*heavy beats*) yanayoambatana na *bass*. Mawazo kama haya yametolewa pia na Suriano (2006 na 2007) na Omari (2009).

Mtazamo mwingine ni ule unaouona muziki wa Bongo Fleva kuwa ni muziki usio na nguzo maalumu. Muziki huu ni tofauti na muziki wa *Hip hop* ambao una nguzo zinazofahamika duniani kote. Nguzo hizo ni pamoja na michoro inayowakilisha maudhui mbalimbali (graffiti), upangaji wa muziki (*deejaying)*, uchezaji wa kujinyonganyonga (*breakdancing),* mshereheshaji (MC) na ughani (*rap)* (Suriano, 2006, 2007; Omari, 2009). Msanii Happiness Thadei (p.h.k Sister P) anazitaja nguzo hizo katika wimbo wake uitwao "MaDJ." Anasema:
(1)

1. Nazo **nguzo tano za *Hip hop*** weka akilini
2. Kwanza naanza na ***DJs*** kuweni makini
3. Pili ***MC*** jiheshimu wacha mapepe
4. Usilete mambo ya ajabu kuwafanya watu wacheke
5. Nayo ya tatu **tungo zako sharti ujumbe zibebe**
6. Zielimishe jamii ili utakacho waelewe
7. Tungo zako zikubalike zitumike hata kwenye mashule
8. ***Breakdance*** nayo mtindo wetu wakati ule
9. Hili ndilo darasa nakupa *Hip hop* shule
10. *Hip hop* nguzo ya tano **michoro**

**Chanzo:** Omari (2009:273)

Kundi la mwisho katika mkanganyiko huu ni la watu ambao wanauona muziki wa Bongo Fleva na *Hip hop* kuwa ni kitu kimoja. Mtazamo huu unadai kuwa hakuna tofauti yoyote kati ya muziki wa aina hizo mbili na hivyo mwanamuziki fulani anaweza kutambuliwa kama mwanamuziki wa Bongo Fleva na pia anaweza kutambuliwa kama mwanamuziki wa *Hip hop*. Mtazamo huu unaonekan`a hata miongoni mwa wasanii wenyewe. Katika utafiti uliozaa

[1] P.h.k inatumika kama kifupi cha `pia hujulikana kama'. Tunatumia kifupi hiki badala ya a.k.a (Hujulikana kama) ambayo imekuwa ikitumika kwa muda mrefu. Hata hivyo bado tunaona matumizi ya vifupisho vyote ni sahihi isipokuwa tu ni vema kutumia kifupisho kimoja katika kazi nzima ili kuepuka mkanganyiko.

makala haya, tulipojaribu kuwauliza baadhi ya wasanii ili kujua mtazamo wao juu ya wasanii fulanifulani kama ni wasanii wa Bongo Fleva au *Hip hop* tulipata majibu ya kutatanisha. Kwa mfano, kuhusu Joseph Haule (p.h.k Profesa Jay/Prof. Jay) na Selemani Msindi (p.h.k Afande Sele), watu walituambia kuwa hao ni wanamuziki wa Bongo Fleva wakati wengine walituambia ni wasanii wa *Hip hop*. Hii inatupa picha kwamba muziki wa Bongo Fleva na *Hip hop* unaonekana kuwa kitu kimoja au kuna kutoelewa ni upi hasa mpaka wa muziki huu.

Ili kuepuka mkanganyiko usio wa lazima, utafiti huu hauna lengo la kujiingiza katika mjadala huo na hivyo katika makala haya muziki wa Bongo Fleva utaitwa pia muziki wa *Hip hop* au wa kizazi kipya. Kwa hali hiyo katika makala haya dhana za Bongo Fleva, *Hip hop* na muziki wa kizazi kipya zitatumika kama visawe.

## 2.0 Madai kwamba Muziki Bongo Fleva Unapotosha Jamii

Madai ya kwamba Bongo Fleva inapotosha jamii yameanza sambamba na kuanza kwa muziki wenyewe. Samwel akichambua maelezo ya Chachage (2002), Suriano (2006) na Omari (2009) anabainisha kwamba muziki wa Bongo Fleva umepingwa na watu wa kada mbalimbali kwa madai kwamba unapotosha jamii. Turejelee anaposema:

> Wanataaluma, wanajamii, waandishi wa habari na wanaharakati mbalimbali wa kidini na kimaadili wamekuwa wakiupinga sana muziki wa Bongo Fleva na kuuhusisha na uhuni, mmomonyoko wa maadili na athari za utamaduni wa Kimarekani. Baadhi ya mambo yanayotumika kuushambulia muziki huu ni mavazi ya wasanii wa Bongo Fleva, lugha wanayoitumia na hata mashairi yao (Samwel, 2011:1).

Miongoni mwa mambo yanayoifanya Bongo Fleva ionekane inapotosha jamii kwanza ni tabia za wasanii wa muziki huu; pili, uvaaji wa wasanii na wanenguaji wao; tatu, maudhui ya muziki huu; nne, lugha inayotumika katika muziki huu na; tano, wasanii wenyewe wa muziki huu (Omari, 2011; Samwel, 2011). Labda tuchambue kwa kina kila sababu kati ya hizi ili tuweze kujenga vema hoja zetu.

Kwa kuanza na tabia za wasanii wa muziki huu, tunaona kwamba kwa kiasi kikubwa wasanii wa muziki wa Bongo Fleva wana tabia zisizokubalika katika jamii. Tabia hizo ni pamoja na uvutaji wa bangi, utumiaji wa madawa ya kulevya na unywaji wa pombe na vileo vingine (Musa, 2011). Tabia hizi, kwa ujumla hazikubaliki katika jamii na hivyo jamii inawaona wasanii hawa kuwa si

mfano wa kuigwa. Aidha, wanamuziki hawa pia wamekuwa wakijiingiza katika vitendo vya uasherati na hivyo jamii kuwaona kuwa watu wasio na mwenendo unaokubalika (Kitangoma, 2011).

Sababu ya pili inayoufanya muziki wa Bongo Fleva kuonekana unapotosha jamii ni uvaaji wa wasanii wa muziki huu pamoja na wanenguaji wao. Kwa kiasi kikubwa wasanii wa muziki wa Bongo Fleva, hasa wanawake, wamekuwa wakivaa mavazi yanayodhalilisha. Mavazi hayo yanaacha sehemu kubwa ya miili yao kama vile mapaja, matiti na kifua wazi. Kutokana na mavazi haya, wanajamii wanauona muziki huu kuwa unaipotosha jamii. Kwa upande wa wanaume nao wanaonekana kuvaa mavazi ya kihuni kama vile suruali ambazo zimechanikachanika au zimejazwa viraka, mlegezo[2] na aina nyingine za uvaaji ambazo si za kistaarabu (Samwel, 2012).

Aidha sababu nyingine ni maudhui ya muziki huu. Kwa kiasi kikubwa maudhui ya muziki wa Bongo Fleva yanaonekana kusifia mapenzi, ulevi na ujambazi (Omari, 2009; Shirima, 2010) na mambo mengine yasiyokubalika na kupuuzia mambo muhimu katika jamii. Mapenzi yanavyosawiriwa katika muziki huu yanasemwa kuwa yako bayana sana na hayana kificho (Samwel, 2011). Mfano mzuri wa nyimbo za Bongo Fleva zinazosawiri hali hii unaonekana katika data namba (3) na (4) kama tulivyonukuu hapa chini:
(3) Wimbo "Nimefika" wa Zainabu Lupangile (p.h.k Zay B) akimshirikisha Complex:

1. Kwenye nanii we mama balaa
2. Una *style* toka umakondeni[3]
3. Mtambo wako ni wa kusoo
4. Wangu wa ujuzi unanifikisha *full dose*
   **Chanzo:** Omari (2011:166)

[2] Samwel (2012b) anaueleza uvaaji huu kuwa ni ule ambao suruali huvaliwa na kuacha nusu ya makalio yakiwa nje. Mtindo huu anaueleza kwamba uliigwa kutoka katika mtindo wa uvaaji uliotumiwa na wafungwa wa Marekani ambao, ili kukwepa wasijinyonge, walinyang'anywa mikanda wakiwa gerezani na hivyo suruali zao kushuka chini na kuacha nusu ya matako yakiwa nje. Wafungwa wengi kati ya hawa walipotoka ndio wakajiingiza katika muziki na kuendelea na uvaaji wao wakijionyesha kwamba wao ni watu waliostahimili shida za gerezani (wagumu). Wanamuziki wa Tanzania nao wakaiga mtindo huo kama walivyoiga vionjo vingine vya muziki wa *Hip hop* wa Kimarekani.

[3] Wamakonde ni watu waishio katika mikoa ya Kusini mwa Tanzania. Watu wa kabila hili wanahusishwa na ujuzi mkubwa wa kufanya mapenzi kutokana na mila ya jando na unyago ambayo inawasaidia kujifunza, zaidi ya mambo mengine, mitindo mbalimbali ya kufanya mapenzi.

Hapa tunaona Zay B anamsifia Complex kwamba anajua sana kufanya mapenzi na anamridhisha. Neno “mtambo” linalotumika hapo linamaanisha “uke” na “full dose” linatumika kumaanisha kuridhika (Omari, khj.). Hivyo katika ubeti huu msanii anasifia ujuzi wa kufanya mapenzi wa mpenzi wake.
(4) Wimbo “Party East Zoo” wa Mez B akiwashirikisha East Zoo

1. ***Mangwair:*** Norah eti amelala kwa Flora
2. Dogo punguza mikasi
3. ***Norah:*** Sitaki mbona nawe unapenda nyasi
4. ***Mangwair:*** Natoka Mbeya hadi East Zoo
5. Napita maskani kupata majani
6. Kisha nakwenda *kumcheck honey*
7. Kiwanjani nakutana na maduu...

**Chanzo:** Omari (2011:164)

Katika ubeti huu tunaona kuna majibizano baina ya wasanii wawili, Albert Ngwea (Mangwair) na Norah. Mangwair anajaribu kumuonya Norah aache tabia ya kuwa na uhusiano na wanawake wengi (*mikasi)* lakini Norah anashangaa kuonywa na Mangwair kwani naye anapenda bangi (majani/nyasi). Mangwair anaonekana katika ubeti huu akisifia bangi kwamba ndiyo inamwezesha kufanya safari za kimuziki (taz. Mstari wa 4). Mangwair anajigamba waziwazi kwamba anaenda kuvuta bangi (mstari wa 5). Aidha, tunaona katika mstari wa 6 na wa 7 Mangwair, zaidi ya kuwa na mpenzi wake (*honey*) bado ana uhusiano wa kimapenzi na wanawake (*maduu*) wengine. Katika beti hizi mbili tunaona kwamba maudhui yanayosawiriwa ni kusifia uwezo wa wapenzi kufanya mapenzi, kusifia kuwa na wapenzi wengi na uvutaji wa bangi.

Katika jamii za Kiafrika masuala ya kingono yanachukuliwa kuwa ni ya siri (Ayisi, 1962; Mair, 1979; Van Pelt, 1971). Hivyo, kwa wasanii hawa kuyaweka hadharani mambo kama: jinsi wanavyofanya mapenzi, jinsi wanavyokata viuno wakiwa kitandani, jinsi wanavyonyonyana ndimi (*kupigana denda*), jinsi wanavyolewa na kufanya vitendo vya aibu na kadhalika kunaonekana kuwa ni kukiuka maadili ya Kitanzania na ya Kiafrika kwa ujumla wake. Aidha, matumizi ya madawa ya kulevya, ikiwa ni pamoja na bangi ni kinyume cha sheria za nchi. Hivyo mambo haya huufanya muziki huu kuonekana kuwa ni wa kihuni na unaopotosha jamii, hasa watoto na vijana.

Vilevile, matumizi ya lugha yanaufanya muziki huu uonekane unapotosha jamii. Kwa kiasi kikubwa, lugha inayotumika katika muziki wa Bongo Fleva ni ya vijana au lugha ya kihuni kama inavyoitwa na wengine. Lugha hii imejaa

misimu na misemo ya mitaani, ambayo wakati mwingine haieleweki kwa watu wengine ambao hawajaizoea (Majembe, 1998; Remes, 1998; Omari, 2011).

Sababu ya mwisho ambayo tutaipitia hapa ambayo inaufanya muziki wa Bongo Fleva uonekane unapotosha jamii wasanii wenyewe wa muziki huu. Kwa kiasi kikubwa wasanii wa muziki wa Bongo Fleva ni vijana ambao wamekuwa wakionekana ni wahuni tu. Aidha, wengi kati ya wasanii wake ni vijana walioacha shule na kujiingiza katika muziki. Hivyo, jamii inaona kuwaunga mkono vijana hawa ni kuhimiza uendelevu wa tabia zao zisizokubalika. Kutokana na haya, muziki wa Bongo Fleva kwa kiasi kikubwa umekuwa ukichukuliwa kama ni muziki unaopotosha. Swali linabaki kuwa je, hoja hizi zina msingi wowote? Kipengele kinachofuata kitachambua hoja hizi.

**3.0 Je, ni Kweli Bongo Fleva Inapotosha Jamii?**

Makala haya yanaona kwamba sababu hizi tano zinazoufanya muziki wa Bongo Fleva kuwa unapotosha jamii hazina mashiko yoyote na ni vigumu kwa wanafasihi kuzitegemea. Tukianza na sababu ya kwanza, tabia za wasanii wa muziki huu, tunaona kwamba ni sababu dhaifu sana kuitumia. Suala la tabia ya wasanii tunaliona kuwa si hoja ya kuitumia kuuhukumu muziki huu. Kwanza izingatiwe kuwa si wasanii wote wa Bongo Fleva wana tabia zinazosemwa hazifai. Wapo wengine ambao hawavuti bangi, hawatumii madawa ya kulevya, hawanywi pombe wala kutumia kilevi chochote. Vilevile wapo ambao hawashiriki ovyo matendo ya ngono bali wameoa au kuolewa na wanaishi vema na wanzi wao.

Katika utafiti uliozaa makala haya tumebaini kwamba kuna wasanii kama Banana Zoro, Malima Lawrence (Marlow), Haroun Kahena (Inspekta Haroun) na Judith Wambura (Lady Jaydee) ambao wameoa na kuolewa na ndoa zao ni mfano mzuri wa kuigwa katika jamii. Tofauti na wasanii wengine ambao huandikwa sana katika vyombo vya habari wakihusishwa na tabia za ngono na kubadilisha wanawake. Hili linathibitishwa na mwandishi wa habari maarufu nchini Tanzania anayewafuatilia sana wasanii, Millard Ayo, anaposema hawa ni mfano wa kuigwa. Millard Ayo anawataka wasanii wengine kuiga mfano wa wasanii hawa.[4] Hivyo, si halali kuwahusisha wasanii wote wa Bongo Fleva na tabia mbaya. Kama tunawatumia wachache wenye kile kinachoitwa tabia mbaya kuuhukumu muziki huu, kwa nini, kwa upande mwingine tusiwatumie wale wachache wenye tabia nzuri kuuhukumu muziki huu? Jambo la kukumbuka ni kwamba wapo askari polisi, wanajeshi, walimu na watu wa taaluma mbalimbali

[4] Habari hii imesomwa katika http://millardayo.com/diamond-platnums-aamua-kutangaza-mpenzi-wake-wa-sasa-ndio-huyu/

ambao wana tabia hizo zinazoonekana kuwa tabia mbaya lakini hatuzihusishi taaluma zao na tabia hizo mbaya. Aidha, wapo pia viongozi wa dini kama vile wachungaji, mapadre na mashehe ambao wana tabia hizo lakini hatuzihukumu dini zao kwa tabia zao. Hili linathibitishwa na msanii wa Bongo Fleva aitwaye Ibrahimu Mohamed (p.h.k Roma) katika wimbo wake uitwao "Mathematics" kama tunavyounukuu hapa chini:

(5)

1. ...Unahitaji kupiga goti mbele ya *altare*
2. **Imamu akizini Njagoa usiukimbie msikiti**
3. **Padri akilala na *Sister* haibadilishi ukatoliki**
4. Hata *gangster* hulegeza macho ukimpa *cotton pads*
5. Mnawakamata mateja wakati nyi ndo mnauza *drugs*
6. Ili ujue fegi imewaka lazima upige pafu
7. So baba usimtume mtoto aiwashe utamuua mapafu
8. Popote umuonapo ng'ombe hapakosi Mmasai
9. Pongwe ndo ngome kongwe Zanzibar usinitoe nishai
10. **Ndoto zangu kitambo zilikuwa nije kuwa padri**
11. **Zikayeyuka nilipopuliziwa moshi wa *weed***
12. **Naenda *church* naanguka tena nasali**
13. Na popote utakaponiona shingoni nimevaa rozali

**Chanzo:** Roma (2011), "Mathematics"

Katika shairi hili tunaona msanii Roma anabainisha wazi kwamba shehe au padre akizini haimaanishi dini nzima imezini (mstari wa 2-3). Aidha, anabainisha kwamba yeye zaidi ya kuwa anatumia bangi (*weed*) lakini bado ana tabia njema na anakwenda kanisani. Hii ina maana kwamba anajaribu kubainisha ukweli halisi kuwa si wote waendao makanisani na misikitini wana tabia mbaya. Hapa msanii anawasilisha wazo linalothibitika hata katika misemo ya Kiswahili kwamba "hakuna binadamu aliyekamilika."

Hivyo tunaweza kusema kwamba, japokuwa makala haya yanatambua kwamba msanii anapaswa kuwa kioo cha jamii kama anavyoimba Selemani Msindi (p.h.k Afande Sele) katika wimbo wake uitwao "Darubini Kali," bado tunaona kwamba msanii kuwa kioo cha jamii ni muhimu lakini pia msanii anapaswa kuyamulikia yale yanayotokea katika jamii. Fasihi ni zao la jamii na hivyo nyimbo za wasanii zinapaswa kusawiri maisha halisi ya jamii. Hili si suala la tabia zao bali maneno yao. Tazama ubeti huu katika wimbo wa "Kioo cha Jamii" Afande Sele anaposema:

(6)

**Kiitikio**

1. Mimi ni msanii x 2 kioo cha jamii x 2
2. Mimi naona mbali x 2 kwa darubini kali x 2

**Ubeti wa 1**

3. ...wasanii muweke akilini hasa kwa mtu makini kiusanii
4. Ila kama mtalii muziki uweke kapuni watakuokota chini
5. Unafanya muziki Bongo unaact kama mamtoni
6. Ya nini bora kuimba katuni lugha ngeni za nini kwenye muziki nyumbani?
7. Wakati Bongo Fleva inapendwa zaidi Uswahilini?
8. Mi nacheka sana kuna vitu vya kuimba vyenye maana kila kona
9. Sasa inakuwa vipi unatajataja majina tu nyimbo nzima?
10. Tena kwa mistari isiyo na vina!

**Ubeti wa 2**

11. Ras naona mbali kwa darubini kali
12. Ndo maana muziki wangu unaegemea kwenye ukweli
13. Kwa mfano labda ungewapa mfano kabla hujashusha kibano
14. Nasema *rap* ni ukweli mtupu
15. Rap kiasili *rap* si kuimba uongo kama siasa za Bongo
16. Useme kwenu una benz wakati nyumba ya udongo
17. Bwana mdogo wacha upambe tu
18. Unapopelekwa tu unakwenda kama ling'ombe
19. Simama utoe ujumbe kama huwezi unyamaze
20. Nasema mara ya mwisho si lazima wote tuimbe

Hivyo tuhitimishe tu kwamba tabia za wasanii wa nyimbo za Bongo Fleva hazitoshelezi kuwa sababu muhimu za kuuchukulia muziki na muziki huu kwa ujumla kwamba ni wa upotoshaji. Tabia ni hulka ya mtu binafsi na haihusiani kabisa na kile anachokifanya.

Sababu ya pili tuliyoibainisha ni uvaaji wa wasanii wa muziki huu na wanenguaji wao. Hii nayo si sababu ya msingi. Ikumbukwe kwamba kila utanzu wa fasihi huwa na aina yake ya uvaaji ambayo huweza kuwa tofauti na uvaaji tuliouzoea katika jamii. Kwa mfano, Rubanza (1994:2) akielezea mavazi katika majigambo ya Kihaya anasema kwamba:

> Pamoja na kujinadi kwa matendo yake, **mjigambi huvaa mavazi maalumu ambayo yanaambatana na tukio hilo la kujigamba**. Mavazi hayo ni pamoja

> na kanzu ndefu na mashuka yanayovaliwa kwa namna maalumu kwa kazi hiyo (msisitizo wangu).

Shuka hizi zinazotajwa na Rubanza zilikuwa nyeupe na zilivaliwa kwa mtindo wa lubega pamoja na kofia (*galushanda* au *pama*). Hapa tunabainishiwa wazi kwamba katika majigambo ya Kihaya kulikuwa na mavazi maalumu ambayo ni tofauti na mavazi ya kawaida. Hili linafafanuliwa na Mulokozi (2002) ambaye anaeleza kwamba mavazi yanayoelezwa na Rubanza hapa ni ya hivi karibuni (karne ya 20). Kabla ya hapo mavazi kama kanzu au shuka hayakuwapo. Mulokozi (2002) anaeleza kwamba mavazi ya jadi ya jamii za Kihaya ni yale yaliyotengenezwa kwa magome ya miti na ngozi za wanyama. Mavazi haya ndiyo yanayoelezwa kutumika katika jamii mbalimbali za Kiafrika (Van Pelt, 1071; Koponen, 1988). Hivyo, mavazi asilia yaliyovaliwa katika majigambo ni mavazi ya ngozi (*ebeebo*) na mirumba (*olubugo*). Hata uvaaji wa lubega uliofuata baadaye uliiga mavazi haya ya asili (taz. uvaaji wa *ebeebo* katika Mulokozi, 2002). Naye Songoyi (2005) anabainisha kwamba hata wasanii wa ngoma za Kisukuma zilizoitwa *Wigashe* walikuwa na mavazi maalumu ambayo ni tofauti na mavazi ya kawaida. Katika jamii za Kisukuma wasanii wa ngoma hizo walivaa mavazi maalumu yaliyoitwa *maleba*.

Mavazi haya yaliyovaliwa katika tanzu mbalimbali za fasihi simulizi, wakati mwingine yalivaliwa yakiacha sehemu kubwa ya miili ya wasanii ikiwa wazi. Kwa mfano, mavazi yale yaliyozoeleka katika ngoma nyingi ambapo wasanii huvaa namna fulani ya matete/ukindu yaliyounganishwa na kamba kuzunguka kiuno yaliweza kuacha sehemu kubwa ya miili yao nje. Pia, kuna baadhi ya aina za wachezaji ngoma walivaa (na bado wanavaa) mavazi ambayo yanafunika sehemu za siri za mbele tu na kuacha sehemu za nyuma zikiwa wazi. Hali hii hutegemeana na utamaduni wa jamii husika. Tunaona hata Wamasai wanavaa shuka moja ndefu sana ambayo huweza kuacha baadhi ya maungo yao ya siri wazi. Uvaaji huu hata hivyo hauhusishwi na upotoshaji wa maadili. Kama ni hivyo kwa nini muziki wa Bongo Fleva unapojitofautisha kwa aina yake ya uvaaji uhusishwe na upotoshaji wa kimaadili?

Sababu nyingine inayotumika kuuhukumu muziki wa Bongo Fleva kama muziki unaopotosha jamii ni lugha inayotumika katika muziki huu. Muziki wa Bongo Fleva, kwa kiasi kikubwa, unatumia lugha ya vijana. Lugha hii inajumuisha lugha mchanganyiko na misimu (Omari, 2009, 2011; Samwel, 2012). Mchanganyiko wa Kiswahili na Kiingereza na mchanganyiko wa Kiswahili na lugha nyingine za makabila, unatumika sana katika muziki wa Bongo Fleva. Majigambo ya Bongo Fleva yana matumizi ya mchanganyiko wa Kiswahili na lugha nyingine za makabila. Hii inatokana na ukweli kwamba

wasanii wa majigambo haya wana makabila yao ambayo wangependa kujitambulisha kwayo (Samwel, khj.). Uchanganyaji wa aina hii unaonekana katika wimbo wa “Walimu” ulioimbwa na Wagosi wa Kaya kama unavyonukuliwa katika data namba (7) hapa chini:

(7)

1. *Goodmorning teacher, goodmorning sir*
2. **Monika zeze** mwalimu hicho ni Kisambaa
3. Nimechanganyikiwa mpaka naongea Kisambaa darasani
4. Na hii ni kwa sababu sina kitu mfukoni

   **Chanzo:** Wagosi wa Kaya (2003), *Ripoti Kamili*

Hapa tunaona zaidi ya uchanganyaji wa Kiswahili na Kiingereza katika mstari wa 1, kuna uchanganyaji wa Kisambaa na Kiswahili katika mstari wa 2. Kirai *Monika zeze* kina maana ya habari za asubuhi katika lugha ya Kisambaa. Uchanganyaji unaonekana pia katika wimbo wa Suma Lee, “Hakunaga,” ambapo msanii anaanza kwa ghani za kikabila. Aidha, hata neno “hakunaga” analolitumia mara kwa mara ni neno lenye asili ya lugha za makabila na hasa Kisukuma. Matumizi haya ya lugha za kikabila yana lengo la kupata soko katika mikoa na maeneo makabila hayo yanamotumika. Sababu nyingine ya matumizi hayo ya lugha, inaweza kuwa harakati za kujinasua kutoka katika athari za kutoka nje (ukoloni mamboleo) na hasa athari za kiutamaduni. Likithibitisha haya *Fiesta* (2011) linasema:

> Mwanamuziki wa Bongo Fleva ***ambaye anatumia lafudhi ya Kimasai katika kuimba nyimbo zake,*** Abel Loshilaa Motika maarufu kwa jina la Mr. Ebbo amewataka wanamuziki wa Bongo Fleva kujivunia lugha yao sio kupenda kutumia lugha za wenzetu katika nyimbo zao. Akizungumza na *Fiesta*, mwanamuziki huyo mkongwe katika fani hiyo alisema kuwa utamkuta mwanamuziki wa Kitanzania anaimba lugha ya kigeni katika nyimbo zetu bila aibu. ***Msanii huyo anajivunia kila kilicho chake na pia hapendi kuiga bali anapenda kubuni na anapobuni anatoka na vitu vya ukweli***. Mr. Ebbo anasema tatizo la wasanii wa Bongo Fleva ni kuigana, kila msanii angekuwa na ubunifu wake basi ingekuwa rahisi kuuzika sokoni lakini wanapoigana kunakuwa hakuna kitu kipya kwa wasikilizaji (Msisitizo wetu).

Katika dondoo hili mwandishi anatueleza kwamba msanii huyu si tu anatumia lugha ya Kimasai, bali pia anatumia lafudhi ya Kimasai. Hivyo zaidi ya mchanganyiko wa lugha katika maneno kuna mchanganyiko wa lugha katika kuchanganya lafudhi ambapo msanii huweza kutumia lafudhi ya lugha ya Kiswahili na lugha za makabila.

Zaidi ya matumizi ya lugha yenye mchanganyiko wa Kiswahili na lugha za makabila, kuna matumizi ya mchanganyiko wa Kiswahili na Kiingereza. Aina

hii ya mchanganyiko wa lugha, imetumika sana katika majigambo ya Bongo Fleva. Mfano mzuri tunauona katika wimbo wa Gwamaka Kaihula (a.k.a Crazy GK) uitwao "Itikadi Zetu" kama unavyonukuliwa hapa chini:

(8)

1. Huyu mjinga sipendi ujinga katika kazi acha masihara
2. Katika kazi mi nilikwambiaje?
3. Nilikwambia nini?
4. *Get up get up GK East Coast baby*
5. Usishangae tunashika *mashine gun* na tunaingia mpaka ndani
6. Naruka ukuta nazama *straight* mpaka ndani
7. Na kumpasua mtu kichwa m'fulani
8. Natorokea dirishani na baadaye naibukia mtaani
9. Nawakuta mamtoni naipora *Erickson naichange line*
10. Wanausalama wananisaka na kuni*target*
11. Hadi Waitara ananisaka mi *wanted*
12. Dakika mbili mara hao na *wanted*

**Chanzo:** Omari (2009)

Maneno yote tuliyoyawekea hati za mlalo katika mashairi ya Bongo Fleva tuliyoyanukuu, yanaonesha matumizi ya lugha yenye mchanganyiko wa Kiingereza katika Kiswahili.

Hata hivyo, kumekuwa na harakati za wasanii kupinga uigaji wa tamaduni za nje yakiwamo matumizi ya lugha ya Kiingereza katika muziki wa Bongo Fleva. Likisisitiza jinsi matumizi ya Kiingereza katika muziki wa Bongo Fleva yanavyopingwa, *Kitangoma* (2011b) linamnukuu msanii Dayna anaposema,

> " …nawashangaa baadhi ya wasanii wenzetu ambao wamekuwa wakikimbilia kuimba kizungu (*Kiingereza)* na kutukuza lugha za nchi nyingine na kukiacha Kiswahili ambacho kwa sasa kimeanza kutambulika duniani" (Ufafanuzi wetu).

Zaidi ya matumizi ya lugha mchanganyiko muziki wa Bongo Fleva pia unatumia misimu. Omari (2009 na 2011) na Samwel (2012) wanakubaliana kwamba misimu ni maneno yanayozuka katika kipindi fulani cha kihistoria na kutumiwa na kundi fulani la watu na hatimaye huweza kupotea au kusanifiwa na kuwa msamiati. Kuna aina mbalimbali za misimu kama inavyobainishwa na Samwel, miongoni mwa aina hizo ni misimu ya vijana, misimu ya wanajeshi, misimu ya makuli na kadhalika. Misimu inayotumika hasa katika muziki wa Bongo Fleva ni misimu ya vijana na hasa vijana wa mitaani. Matumizi ya misimu hii yanatokana na sababu kuu mbili: kwanza, fanani na hadhira ya muziki wa Bongo Fleva kwa kiasi kikubwa ni vijana na ndiyo maana huitwa

muziki wa kizazi kipya (Suriano, 2006; Omari, 2009; Samwel, 2012). Pili, wasanii wengi wa muziki wa kizazi kipya ni vijana waliokuwa mitaani ambao hawakuwa na kazi ya kufanya na hivyo kuamua kuwa wasanii ili kujikwamua kimaisha (Keyes, 2002; Kisanda, 2010). Akithibitisha hili Kisanda (2010) anasema:

> Uwepo wa muziki wa Bongo fleva, umekuwa na faida kubwa kwa vijana wa taifa hili na kuufanya muziki huo kuchukuliwa kama mkombozi kwa kugeuka ajira kwa vijana, hasa kwenye wakati huu wa maisha magumu na ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana wengi katika taifa hili linalosifika kwa amani na upendo duniani kote.

Suala la muziki wa Bongo Fleva kutoa ajira kwa vijana linajadiliwa kwa kina na Mwanjoka (2011:102-103) anaposema:

> Muziki huu wa kizazi kipya umefanikisha kwa kiasi kikubwa kuwakomboa vijana wengi wa Tanzania waliokuwa kwenye hali mbaya kimaisha. Si wanamuziki tu, bali hata wale waliokuwa sio wanamuziki. Waliopo mijini na vijijini, waliokimbia vijijini kwa ajili ya ugumu wa maisha na kuja mijini, wake kwa waume…tangu mwaka 1998 muziki huu umeanza kutoa ajira hasa kwa wanamuziki, wasambazaji wakubwa na wale wadogo na maarufu kama machinga. Kabla ya muziki huu vijana wengi walikuwa hawana kazi na walikuwa wakishinda vijiweni na kupoteza muda wao kwa kuvuta sana bangi. Na bangi ilivutwa kwa sababu ilikuwa ndio kilevi chenye bei rahisi. Kilevi kama bia kilikuwa ni ghali na waliokuwa wanakunywa ni watu ambao walikuwa na hela za kutosha…muziki huu uliongeza ajira kwa wasambazaji wadogo wadogo (machinga), ajira kwa waandishi wa habari hususan wa makala za wasanii, watangazaji na maDJ katika vituo mbalimbali vya redio na televisheni hata katika kumbi za starehe, baa na hoteli kubwa nchini.

Nukuu hii ya Mwanjoka inathibitisha kwamba wasanii wengi wa muziki huu na wadau kwa ujumla wake ni vijana na kwamba baadhi yao walikuwa wahuni hapo awali wakivuta bangi na kutumia madawa mengine ya kulevya. Hivyo, misimu inayotumika, inajumuisha pia misimu ya kihuni na ya kijiweni. Matumizi haya ya lugha ndiyo yanayoufanya muziki huu kuonekana kuwa ni wa kihuni na hivyo unapotosha jamii.

Hata hivyo kuuchukulia muziki wa Bongo Fleva kuwa unapotosha jamii kwa kigezo cha matumizi yake ya lugha ni hoja dhaifu sana. Tunaona, kwa mfano, matumizi ya lugha mchanganyiko, na hasa mchanganyiko wa Kiswahili na Kiingereza ambayo ndiyo yanayohusishwa na uhuni, si sababu ya msingi. Matumizi ya lugha mchanganyiko yanasawiri hali halisi ya jamii kwani fasihi ni kioo cha jamii. Jamii ya Kitanzania ya leo inatukuza sana lugha ya Kiingereza na kupuuza lugha yake ya Kiswahili. Leo hii anayejua Kiingereza ndiye

anayeonekana kuwa msomi na mjuzi wa mambo. Hata pameanzishwa shule mbalimbali zinazoitwa za kimataifa na zinazotumia lugha ya Kiingereza kama lugha ya kufundishia ambazo hufundisha masomo yote kwa lugha ya Kiingereza (Batibo, 1992). Mtoto anayesoma katika shule hizo ndiye anayeonekana kutoka katika familia bora. Aidha, tunaona matumizi ya lugha mchanganyiko hata kwa viongozi mbalimbali wa serikali ikiwa ni pamoja na wabunge. Hivyo, matumizi haya katika muziki wa Bongo Fleva ni kielelezo tosha kwamba muziki huu unaisawiri jamii na hivyo una faida kubwa kwa jamii husika. Ni tabia ya kazi yoyote ya fasihi kuiakisi jamii husika (Mulokozi, 1996; Samwel, 2012).

Kuhusu matumizi ya misimu nayo si hoja kuntu. Omari (2009 na 2011) na Samwel (2012) wanafafanua kwa kina umuhimu wa misimu katika muziki wa Bongo Fleva. Omari (khj.) anabainisha kwamba muziki wa Bongo Fleva unatumia misimu ya vijana inayohusu dawa za kulevya, wanawake na viungo vya mwili, mapenzi, mavazi, fedha na misimu kuhusu UKIMWI na Kondomu. Omari (khj.) anabainisha kwamba matumizi haya ya misimu katika muziki huu yanasaidia sana kufikisha ujumbe wa nyimbo zao kwa jamii husika na pia ni muhimu katika kuuelewa utamaduni wao kwa ujumla. Aidha, Samwel (khj.) anabainisha kwamba misimu husaidia kukuza lugha, kuepusha migongano na pia hupendezesha nyimbo. Hii ina maana kwamba baadhi ya misimu inayotumika katika muziki huu imesanifiwa na kufanywa misamiati ya Kiswahili. Hata jina lenyewe la muziki huu "Bongo Fleva" lilianza kama msimu lakini leo hii limesanifiwa na linatumika hivyo duniani kote. Aidha, misimu huwafanya wasanii kuimba mambo ambayo vinginevyo wasingeweza kuimba. Tunaona, kwa mfano, kupitia misimu wasanii wanaweza kuwasema viongozi wa serikali bila kuchukuliwa hatua yoyote. Lakini kama wangewasema waziwazi bila shaka wangechukuliwa hatua. Vilevile masuala yahusuyo ngono, UKIMWI na wanawake wasingeweza kuyaimba waziwazi; ilikuwa ni lazima kutumia lugha ya kificho. Hapo ndipo misimu ilipotumika kusaidia hilo. Hivyo, matumizi ya misimu katika muziki huu yana faida kubwa kuliko hasara na hivyo si sahihi kuyachukulia matumizi hayo kama upotoshaji wa maadili ya jamii.

Sababu ya mwisho inayoufanya muziki huu kuonekana unapotosha jamii kama tulivyodokeza hapo awali ni wasanii wenyewe wa muziki huu. Baadhi ya wasanii wa muziki wa Bongo Fleva ni vijana wa mtaani ambao wamekuwa wakionekana ni wahuni tu. Aidha, wengi kati ya wasanii wake ni vijana walioacha shule na kujiingiza katika muziki. Hivyo, jamii inaona kuwaunga mkono vijana hawa katika muziki wao ni kuuunga mkono tabia zao mbaya.

Tabia zao zisizokubalika zinaonekana hata katika mashairi yao ambapo wamekuwa wakijinadi kuwa wao ni malaya majambazi, wauaji, na kadhalika.

Zaidi ya mifano tuliyoiangalia hapo awali, mfano mwingine ni wimbo wa GK tuliounukuu katika data namba (8) hapo juu. Katika wimbo huo msanii anajigamba kwamba yeye ni mwizi na anaiba simu za watu, yeye ni muuaji, na kadhalika.

Hali kama hiyo pia inaonekana katika wimbo wa Zay B uitwao "Gado" tunaona msanii pia anajinadi kwamba yeye ni gaidi na mtu hatari sana. Anaendelea kujigamba kwamba mtu akimchezea atamchinja kama inavyoonekana katika ubeti tuliounukuu hapa chini:
(9)

1. Zay *to the B* **Mwanadada Gaidi**
2. Sitaki ushahidi nini cha ziada
3. Mimi ni *danger* usinichezee ntakuchinja
4. Niko gado[5] tena bado
5. Huwezi kucheza na anga hizi

   **Chanzo:** Omari (2009:333)

Hata hivyo, kuuchukulia muziki huu kwamba ni upotoshaji kwa sababu tu wasanii wengi hawana tabia njema na pia hujinadi hivyo si sababu madhubuti. Kwanza, ifahamike kwamba, kama tulivyoeleza hapo awali, wasanii wengi walikuwa wahuni kabla ya kujiingiza katika muziki huu. Hivyo wanachokiimba kinasawiri maisha yao halisi kabla ya kujiingiza katika muziki huu. Pili, kujinasibisha na tabia kama uuaji na ujambazi ni kutokana na asili ya muziki wenyewe. Omari (2009) anabainisha kwamba muziki huu unasemwa kuchimbuka katika muziki wa *Hip hop* wa Marekani ambapo wasanii wengi huko walikuwa ni watu walioishi maisha magumu na kupitia jela. Hivyo, sifa kubwa ya wasanii wa mwanzo wa muziki huu ni ugumu-kuweza kuvumilia shida. Hiki ndicho wanachojigamba katika muziki huu. Tatu, wanapojigamba kwamba wao ni magaidi, wauaji na wezi ni sitiari tu; wakimaanisha kwamba wao ni watu hatari katika muziki wa Bongo Fleva kama alivyo jambazi au muuaji (Samwel, 2012). Aidha, matumizi ya sitiari hizo yapo hata katika tanzu zingine za kijadi kama anavyobainisha Samwel kwamba katika majigambo ya jadi ya Kihaya, wasanii walijinadi pia kwamba wao ni wezi, majambazi, malaya na kadhalika. Tazama mfano wa jigambo liitwalo "Okwebuga kwa Mugasha" (Kujigamba kwa Mugasha):

---

[5] *Gado* ni msimu ambao unamaanisha `kuwa' imara.

(10)

| | |
|---|---|
| 1. *Nayebuga ndi kijuikanila-nda* | 1. Najigamba *Kijuikanila-nda* |
| 2. *Ky'omwa Lwamula ilembo,* | 2. Kwa *Lwamula ilembo*[6] |
| 3. *Entale Lubologa nsindila omumalungu* | 3. Simba mkali angurumaye mwituni |
| 4. *Ngutula enyama ndaliila* | |
| 5. *Manya bakama bazo tibaija Kyamuyanje* | 4. Hukatakata nyama na kuila |
| 6. *Mba kishuma kyo' Mugasha yahaile* | 5. Najua wenyewe hawaji *Kyamuyanje* |
| 7. *Ekiyo mbanda kabugu, Lubaga* | 6. **Mimi ni jizi aliyepewa kisu kikali na *Mugasha,***[7] |
| 8. *Nyitila enfulu abutumbi* | 7. Kisu kitumikacho kuchinja |
| 9. *Mba kyegile;* | 8. Huulia samaki kilindini |
| 10. *Mba lulabyo, ndabiza kabwela* | 9. Mimi ni mtu asiyeogopa chochote |
| 11. *Omubanyanga ilala itakamile* | 10. Mimi ni radi, humulika kabwela |
| 12. *Abayebembeile nkaita* | 11. Kwa wachezaji ngoma |
| 13. *Abasigaile enyuma echuchu* | 12. Ng'ombe hulala bila kukamuliwa |
| 14. *Yabaigala amaisho* | 13. **Waliotangulia niliwaua** |
| | 14. **Waliobaki nyuma vumbi liliwaziba macho** |
| 15. *Nikwo kyunyeta eibala lya Tibandekile Lwabukaya* | 15. Ndipo waliponibatiza jina la *Tibandekile Lwabukaya* |

**Chanzo:** Rubanza (1994)

Kwa kuhitimisha, tuseme tu kwamba, hakuna sababu ya msingi inayoweza kutumika kuhalalisha madai kwamba muziki wa Bongo Fleva unapotosha jamii au ni muziki wa kihuni. Labda ni kutokana na hilo ndiyo maana leo hii wanajamii kiasi wameukubali muziki huu na tunaona hata ukitumika katika shughuli mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Mwanjoka (2012) anathibitisha kwamba muziki wa Bongo Fleva kwa sasa unatumika katika kampeni za urais, katika kuhamasisha masuala mbalimbali kama vile kupiga kura, amani, vita dhidi ya UKIMWI, na kadhalika. Hata hivyo, hii haimaanishi kwamba wanajamii wote wanaukubali muziki huu.

## 4.0 Madai Haya ni Mapya?

Baada ya kupitia hoja moja baada ya nyingine tumebaini kwamba hakuna hoja madhubuti inayoweza kutegemewa katika kudai kwamba muziki wa Bongo Fleva unapotosha jamii. Swali linabaki kuwa je, madai ya utanzu fulani wa fasihi au fasihi kwa ujumla kupotosha ni madai mapya katika fasihi ya Kiswahili? Katika kipengele hiki tutalishughulikia hilo.

Katika utafiti uliozaa makala haya tumebaini kwamba madai kwamba utanzu fulani unapotosha si mapya na yamekuwapo kwa muda mrefu. Mijadala hii inaonekana katika Nyanyembe (1994); Mulokozi (1996); Omari (2009); Samwel (2011 na 2012) miongoni mwa wengi wengineo. Ni ukweli usiopingika

[6] *Lwamula ilembo* ni usemi wa Kihaya ambao unamaanisha mleta baraka

[7] *Mugasha* ni muungu wa Wahaya anayehusika na ziwa. Katika jamii za Wasukuma huitwa *Ngassa*.

kwamba utanzu wowote wa fasihi unaweza kupotosha kama usipochukuliwa kwa tahadhari au kuzingatia mipaka yake ya utendaji. Katika utanzu wa semi, kwa mfano, tunabaini wazi kwamba methali zinaelimisha sana. Methali kama vile "aliye juu mngoje chini"; "sikio halizidi kichwa"; "wa mbili havai moja"; "haraka haraka haina baraka" na nyinginezo nyingi zinatoa maadili muhimu sana katika jamii.

Tukianza na methali "aliye juu mngoje chini" tunaona kwamba inahimiza wanajamii kuwa wavumilivu na kwamba pale wanaponyanyaswa na kuonewa hawana budi kuwa na subira maana ipo siku wanaowanyanyasa "watashuka chini." Hata hivyo zaidi ya kuelimisha huko, methali hii inaweza kupotosha. Methali hii kwa upande mwingine inawahimiza wanajamii kutochukua hatua pindi mabaya yanapofanywa katika jamii kwa imani kwamba kuna siku mambo yatakaa sawa. Mwelekeo huu kwa hakika ni wa upotoshaji kwani kama wazee wetu wangeichukulia methali hiyo kwa mkondo huo hakuna shaka hadi leo ukoloni ungekuwa bado unaendelea kwani wasingepambana nao.

Hali kama hiyo inaonekana katika methali "sikio halizidi kichwa." Methali hii ni muhimu sana katika kuadilisha. Inajaribu kutoa onyo kwa watoto na wengine kwamba kamwe hawawezi kuwa na hekima kuliko wazee wao. Hivyo inahimiza watoto kuwaheshimu wakubwa wao. Hata hivyo, kama methali hii isipochukuliwa kwa tahadhari inaweza kupotosha jamii. Upotoshaji unaweza kutokana na ufafanuzi kwamba methali hii inadidimiza juhudi katika maendeleo. Methali hiyo inaweza kuchukuliwa kwamba inawaonya watoto kutotia bidii katika kazi kwani kama wazazi wao ni maskini wao kamwe hawawezi kuwa na maisha bora tofauti na wazazi wao.

Kwa upande wa methali ya "haraka haraka haina baraka" tunaweza kusema kwamba inafanana na methali nyingine kama vile "polepole ndiyo mwendo," "subira yavuta heri" na kadhalika. Methali hizi zinaionya jamii kutofanya mambo kwa pupa. Kabla ya kufanya jambo lolote lile ni muhimu kutafakari na kupanga mikakati ya kulifanya jambo husika. Hata hivyo, zaidi ya kuelimisha methali hii inaweza kupotosha na hasa pale inapotumika katika mazingira yasiyofaa. Kwa mfano, kama mtu ana mgonjwa na akatumia methali hii bila shaka mgonjwa huyo atakufa kwani mgonjwa anahitaji huduma ya haraka. Vivyo hivyo, kama mtu amevamiwa na majambazi au anakabiliwa na hatari na akazitumia methali hizi hatuna shaka kwamba atapatwa na madhara makubwa kwani katika nyakati za hatari maamuzi ya haraka huhitajika. Mbali na upotoshaji wote huu bado methali zitabaki kuwa tungo fupifupi za hekima na za kimapokeo zinazotumika kurithisha falsafa ya jamii kutoka kizazi kimoja hadi kingine (Mulokozi, 1996; Cuddon, 1998; Senkoro, 2011).

Uwezekano wa utanzu fulani kupotosha jamii hauishii tu katika semi, na hasa methali bali unaonekana pia katika tanzu nyinginezo. Kwa mfano, jando na unyago zimekuwa zikishambuliwa na wanaharakati mbalimbali kwamba zinapotosha jamii (George, 2010). Miongoni mwa mambo ambayo yamesemwa kupotosha ni pamoja na mafundisho yatolewayo huko, vifaa vitumikavyo kutahiri watu na kadhalika. Kuhusu mafunzo, kwa mfano, wanaharakati mbalimbali wanadai kwamba jando na unyago zinawafundisha masuala ya ngono vijana wadogo na hivyo kusababisha mimba za utotoni na maambukizi ya virusi vya UKIMWI, kwani vijana hao mara watokapo jandoni na unyagoni huweka katika vitendo masuala waliyojifunza huko. Aidha, kuna madai kwamba hata vifaa vinavyotumiwa katika zoezi la kutahiri ni hatarishi na huweza kusababisha maambukizi ya UKIMWI kwani havichemshwi, pia hutumiwa kwa wari wote waliopo jandoni. Zaidi ya ukweli unaoweza kuwapo katika madai haya bado ukweli kwamba jando na unyago ni vitu muhimu sana hauwezi kupingwa. Jando ndiyo mfumo rasmi wa elimu ya Kiafrika ambayo iliwafundisha vijana masuala muhimu kama mila na desturi, majukumu ya kifamilia, kilimo bora, na kadhalika (Van Pelt, 1971).

Tuhitimishe sehemu hii kwa kueleza kwamba utanzu wowote wa fasihi unatimiza majukumu makuu mawili ya kifasihi ambayo ni kuelimisha na kuburudisha (Mulokozi, 1996; Samweli, 2012). Katika kuelimisha ndipo tunaona kuwa kuna mambo kama kuadilisha, kuadibisha, kuonya, kukosoa, kuhifadhi amali za jamii, kuendeleza historia, na kadhalika. Mbali na dhima hizo kuu mbili za fasihi, isipochukuliwa kwa tahadhari, fasihi huweza kuipotosha jamii. Hivyo ni jukumu la wanajamii kuichukulia kazi yoyote ile ya fasihi kwa uangalifu mkubwa ili iweze kuwafaidisha. Aidha, ni jukumu la wasanii wa kifasihi kuhakikisha kadri inavyowezekana kuwa wanatoa kazi bora za kifasihi ambazo zitatimiza majukumu ya kuelimisha na kuburudisha na kupunguza uwezekano wa kupotosha jamii.

## 5.0 Hitimisho

Tunahitimisha mjadala wetu kwa kusema kwamba muziki wa Bongo Fleva, kama tanzu nyingine za fasihi, una dhima kubwa sana kwa jamii inayoutumia. Omari (2009), Mwanjoka (2012) na Samwel (2012), miongoni mwa wengine wanabainisha kwamba muziki huu unatimiza majukumu ya msingi ya kifasihi ya kuelimisha na kuburudisha. Hivyo ni jukumu la wanajamii kuuangalia muziki huu kwa jicho chanya ili uweze kutimiza majukumu hayo.

## Marejeo


Ayisi, E.O. (1972). *An Introduction to the Study of African Culture*, Nairobi: East African Educational Publishers.

Batibo, H. M. (1992). "The Fate of Ethnic Languages in Tanzania." Katika M. Brenzinger (mh.), *Language Death: Factual and Theoretical Explorations with Special Reference to East Africa*, p. 85–95. Berlin: Mouton.

Bongo Celebrity. (2011). http://www.wahapahapa.com iliyopakuliwa tarehe 22/08/2011.

Bynoe, Y. (2006). *Encyclopedia of Rap and Hip Hop Culture*, London: Greenwood Press.

Chachage, C. S. L. (2002). "Ndani ya Bongo: Utamaduni na Migogoro ya Utamaduni." *Paper presented at the Tenth Conference on the Political Environment in Tanzania, 17TH – 18th* September, Dar es Salaam.

Cuddon, J.A. (1998). *Dictionary of Literary Terms and Literary Theory*, Great Britain: Andre Deutsch.

*Fiesta*. (2011). "Mr. Ebbo Alia na Wasanii Wanaopenda Kuiga," Aprili – Mei, 2011, Dar es Salaam: Jamana Printers Ltd, uk. 27.

George, V. (2010). "Wamasai Watakiwa Kuacha Ukeketaji," *Mwananchi*, Tarehe 24 Novemba, 2010, Dar es Salaam: Mwananchi Communicatins Ltd.

Keyes, C. L. (2002). *Rap Music and Street Consciousness*, Urbana: University of Illinois Press.

Kitangoma. (2011a). "Sanaa Imegeuzwa Chombo cha Starehe na Kutukuza Anasa," Aprili – Mei, 2011, Dar es Salaam: PrimeTime Promotions Co. Ltd., uk. 7.

__________.(2011b). "Lugha Yetu ya Taifa ina Vionjo Vingi Wasanii Tuitangaze," Aprili – Mei, 2011, Dar es Salaam: PrimeTime Promotions Co. Ltd., uk. 22-23.

Mair, L. (1979). *African Societies*, Cambridge: Cambridge University Press.

Majembe, A. K. (1998). "Language Use in the Tanzanian Hip hop Scene," Unpublished Research Paper, UDSM.

Mbilinyi, J. (2011). *Sugu*: *The Autobiography, Muziki na Maisha From the Streets to Parliament*, Deiwaka: Dar es Salaam.

Mulokozi, M. M. (1986). "The Nanga Epocs of the Bahaya: A Case Study in African Epic Characteristics," PhD Thesis (Unpublished), Dar es Salaam: University of Dar es Salaam.

___________ (1996). "Fasihi ya Kiswahili," Dar es Salaam: OUT.

__________ (2002). *The African Epic Controversy: Historic, Philosophical and Aesthetic Perspectives on Epic Poetry and Performance*, Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Musa, M. (2011). "Nyota wa Bongo Fleva Aliyeteketea' kwa Cocaine," *Habari Leo*, Tarehe 31, Julai, 2011, Dar es Salaam: TSN Publishers, uk. 14.

Mwanjoka, G. (2011). *Harakati za Bongo Fleva na Mapinduzi*, Dodoma: H.M.

Omari, S. (2009). "Tanzanian Hip hop Poetry as Popular Literature," PhD Thesis (Haijachapishwa), Dar es Salaam: University of Dar es Salaam.

_________ (2011). "The Role of Slangs in Understanding Bongo Fleva Content and Culture," Katika Reading in Ethnomusicology: A Collection of Papers Presented at Ethnomusicology Symposium 2011, University of Dar es Salaam.

Perullo, A. (2003). "The Life that I Live: Popular Music, Urban Practises, and Agency in Dar es Salaam, Tanzania," Ph.D Dissertation, Indian University.

Remes, P. W. (1998). "Karibu Geto Langu/Welcome in My Ghetto: Urban Youth, Popular Language and Culture in 1990's Tanzania," PhD Dissertation, Northwestern University.

Rubanza, Y. I. (1994). *Fasihi Simulizi: Majigambo* (*Ebyebugo*), Dar es Salaam: DUP.

Samwel, M. (2011). "Siasa katika Nyimbo za Mapenzi za Bongo Fleva," Katika Omari, S. na Mrikaria, G. (wah.), *Mulika*, Toleo No. 29 & 30, Toleo Maalumu la Muziki wa Kizazi Kipya.

________ (2012). "Mabadiliko katika Majigambo: Uchunguzi wa Majigambo ya Jadi na ya Bongo Fleva," Tasnifu ya PhD (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Shirima, J. (2011). "Wasanii Watano Wanaosifia Pombe," *Ijumaa*, Tarehe 21 Juni 2011, Dar es Salaam: Jamana Printers, uk. 3.

Suriano, M. (2006). **"**Hip hop and Bongo Flavour music in Contemporary Tanzania: Youths' Experiences, Agency, Aspirations and Contradictions", Paper submitted for the conference, "Youth and the Global South: Religion, Politics and the Making of Youth in Africa, Asia and the Middle East", Dakar, 13–15 October 2006.

_________ (2007). "*Mimi ni Msanii, Kioo cha Jamii*, Urban Youth Culture in Tanzania as Seen Through *Bongo Fleva* and Hip- Hop," *Swahili Forum* 14 (2007): 207-223.

Van Pelt, P. (1971). *Bantu Customs in Mainland Tanzania*, Tabora: T.M.P Book Department.